

# **HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM**

## **BARUA ZOTE ZIPELEKWE KWA MKURUGENZI WA JIJI**

S.L.P : 9084  
SIMU : 2123551/5  
FAXI : 2125589  
BARUA PEPE : cd@dcc.go.tz



**UKUMBI WA JIJI**  
**1 BARABARA YA MOROGORO**  
**11882 DAR ES SALAAM**

**05 Februari, 2016**

## **TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imepanga kutumia kiasi cha Shilingi Milioni Mia Tano kutekeleza mpango wa kuboresha huduma za usafi wa mazingira ulioandaliwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa Mkoa wa Dar es Salaam. Katika utekelezaji wa mpango huo endelevu, eneo maalumu litakalojulikana kama "Smart Area" linaloundwa na maeneo kutoka Manispaa za Ilala, Kinondoni na Temeke limekwishaainishwa. Utekelezaji wake utasimamiwa na Mkurugenzi wa Jiji na kuratibiwa na Katibu Tawala Mkoa wa Dar es Salaam ikihusisha maeneo yafuatayo:

- (1) Kuanzia makutano ya Barabara ya Uhuru na Kawawa hadi eneo la Morocco.
- (2) Barabara ya Ali Hassani Mwinyi- kuanzia eneo la Morocco hadi Daraja la Sarenda kuelekea fukwe za Ocean Road, Kifukoni, Bandari hadi makutano ya Barabara ya Kilwa na Mandela (eneo la Uhasibu) na Barabara ya Nyerere na Mandela (eneo la Tazara).
- (3) Kuanzia makutano Barabara ya Nyerere na Mandela (eneo la Tazara) hadi makutano ya Barabara ya Kawawa na Uhuru.
- (4) Maeneo ya kiutalii-maeneo yote ya fukwe.
- (5) Njia kuu za mapokezi ya wageni-Barabara ya Nyerere kuelekea Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Barabara ya Mwai Kibaki hadi Hoteli ya Whitesands kupitia Barabara ya Mbezi Chini.
- (6) Barabara ya Morogoro na Barabara zote za Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka (Dar es Salaam Rapid Transit (DART)).

Mpango huo utakapoanza kutekezwa biashara zisizo rasmi, bodaboda, guta na mikokoteni hazitaruhusiwa katika "Smart Area." Majengo chakavu na mabovu hayatahitajika, utupaji wa taka ovyo na matumizi ya maeneo yasiyo rasmi kwa ajili ya kukusanya taka yatadhibitiwa kwa kufuata na kusimamia sheria. Mambo mengine yasiyotakiwa

katika eneo hilo ni omboaomba, wamachinga kufanya biashara za mikononi, wafanya biashara zilizosajiliwa hawataruhusiwa kupanga biashara nje ya maduka yao, kuwasha moto na kupika katika maeneo yasiyo rasmi.

Gereji bubu, “Show Rooms” za magari katika makazi ya watu, uegeshaji ovyo wa magari, kujisaidia na kutema mate ovyo ni shughuli ambazo hazitaruhusiwa kabisa katika eneo hilo. Pamoja na shughuli hizo zingine ni zisizoruhusiwa ni kuwa na mabango yaliyochakaa kwenye vituo vyta mabasi, nyumba au majengo kutumiwa bila kuwa na “pavements” zilizojengwa kitaalam. Kubandika matangazo bila kibali maalumu, kuunganisha mfumo wa maji taka kwenye mifereji ya wazi ya maji ya mvua ni sehemu ya shughuli zinazozuiliwa pia katika eneo. Uoshaji wa magari katika maeneo yasiyo rasmi katika eneo la “Smart Area”, kusababisha kelele na kupiga muziki kwa sauti kubwa bila kupata kibali pamoja na kuingiza malori zaidi ya tani 10 bila kibali pia ni mambo yaliyomo katika orodha ya shughuli zilizopigwa marufuku kufanyanyika katika eneo hilo.

Kwa taarifa hii, Halmashauri ya Jiji inatoa rai kwa wananchi kuanza kufanya maandalizi ya kushirikiana na mamlaka zao katika utekelezaji wa mpango huo. Maeneo mengine yasiyotajwa katika “Smart Area” yataendelea kusimamiwa na mamlaka husika kwa mujibu wa sheria na wananchi wote waendelee kushiriki katika shughuli za usafi katika maeneo hayo.

Imetolewa na:

Gaston Makwembe  
Mkuu wa Kitengo cha Itifaki na Uhusiano na Umma  
**HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM**  
05 Februari, 2016